

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**  
(BARUA ZOTE ZIPELEKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI)



Tarehe: 03 Septemba, 2020

## **TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUEPUKA MATAPELI KATIKA ENEO LINALOJENGWA KITUO KIPYA CHA MABASI KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM**

Kutokana na taarifa iliyotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya kuwahamasisha Wananchi kujiandaa kutumia fursa za biashara mbalimbali katika Kituo kipya cha kisasa cha mabasi ya abiria, chenye hadhi ya Kimataifa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, kinachojengwa katika eneo la Mbezi Luis Jijini Dar es Salaam, wananchi wengi wanafika katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam wakiwa na maelezo waliyopata kabla ya taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam tarehe 24 Agosti, 2020 wakielezea taratibu walizokwishapata kutoka kwa **watu ambao sio Watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.**

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inarudia kuwasisitiza wananchi kwamba taarifa zote sahihi kuhusu upatikanaji wa huduma hizo zinatolewa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kupitia vyombo mbalimbali vya habari, mbao za matangazo na tovuti ya Halmashauri kupitia anuani [www.dcc.go.tz](http://www.dcc.go.tz). Wananchi wote wanaojiandaa kufanya biashara katika kituo hicho baada ya kutangazwa kwa zabuni na kupatikana washindi wa zabuni zitakazotangazwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Zabuni wanasisitizwa kuepuka matapeli katika eneo la ujenzi wa kituo hicho na kupuuzia maelekezo waliyoyapata kutoka kwa watu hao wasiohusika. Aidha, wananchi wanakumbushwa kwamba maombi yanayotumwa katika kipindi hiki kabla ya tangazo la Zabuni hayatafanyiwa kazi. Tafadhali wajulishe na wengine kuepuka kutapeliwa.

Sipora J. Liana  
**MKURUGENZI WA JIJI.**